



## TAARIFA KWA UMMA

### KUFUTWA KWA LESENI ZA KUFANYA BIASHARA YA KIBENKI KWA BENKI ZA COVENANT BANK FOR WOMEN (TANZANIA) LIMITED, EFATHA BANK LIMITED, NJOMBE COMMUNITY BANK LIMITED, KAGERA FARMERS COOPERATIVE BANK LIMITED NA MERU COMMUNITY BANK LIMITED NA KUWEKWA CHINI YA UFILISI

Kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 56(1)(g), 56(2) (a), (b) na (d), 58(2)(i), 11(3)(c) na (j), 61(1) na 41(a) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, Benki Kuu ya Tanzania imeamua kuzifunga; kusitisha shughuli zake zote za kibenki; kufuta leseni zake za biashara ya kibenki; na kuziweka chini ya ufilisi benki zifuatazo:

1. Covenant Bank For Women (Tanzania) Limited,
2. Efatha Bank Limited,
3. Njombe Community Bank Limited,
4. Kagera Farmers' Cooperative Bank Limited; na
5. Meru Community Bank Limited.

Aidha, kwa mamlaka iliyopewa chini ya kifungu Na. 41(a) cha Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006; BENKI KUU YA TANZANIA imeiteua BODI YA BIMA YA AMANA (The DEPOSIT INSURANCE BOARD) kuwa mfilisi kuanzia tarehe 04 Januari 2018.

Uamuzi huu umechukuliwa baada ya Benki Kuu ya Tanzania kujiridhisha kuwa benki hizi zina upungufu mkubwa wa mtaji kinyume na matakwa ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Upungufu huo wa mtaji unahatarisha usalama wa sekta ya fedha, na kwamba kuendelea kutoa huduma za kibenki kwa benki hizo kunahatarisha usalama wa amana za wateja wake.

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kuuhakikishia umma kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenyewe amana katika mabenki kwa lengo la kuleta uhimilivu katika sekta ya fedha.

**BENKI KUU YA TANZANIA**  
**04 Januari 2018**